

MUHTASARI WA UTAFITI WA AWALI KUHUSU Pembejeo Feki Wilayani Mbozi



Kituo cha Utafiti wa Sera na Utetezi (CPRA), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

1.0 Utangulizi

Takribani asilimia 70 ya Watanzania hutegemea kilimo kwa chakula chao na ustawi wao kijamii na kiuchumi. Hata hivyo, ustadi katika kuzalishaji wa mazao ni wa chini mno. Pamoja na hitihada za kuboresha kilimo nchini Tanzania, hatujafanikiwa sana kutokana na changamoto mbalimbali. Miongoni mwa changamoto hizo ni matumizi ya pembejeo zisizosahihi. Nyingi ni bandia au zimefifishwa. Hatua zinazochukuliwa na vyombo mbalimbali kudhibiti hali hii, hazijafanikiwa vya kutosha, aidha hakuna nyaraka / machapisho yanayoelezea hali halisi. Ni kwa sababu hii ACT kwa kushirikiana na wabia wake, ilichukua jukumu la kuchunguza undani wa suala hili wilayani Mbozi ikijumuisha na wilaya mpya ya Momba.

Pembejeo zinazochakachuliwa sana kwenye mlolongo wa thamani ni: mbegu bora, mboleana viuatilifu. Inakisiwa kwamba nchini Tanzania zaidi ya asilimia 40 ya pembejeo zinazouzwa na kutumiwa na wakulima sio halisi. Hali ni mbaya zaidi kwa wakulima wadogo ambao wengi wao hawana uwezo kifedha na kielimu. Ndiyo sababu huwa wahanga kwa zaidi ya asilimia 80.

Ni ukweli usio na shaka kwamba pembejeo zilizohalisi huongeza mavuno, hivyo kuchangia kuboresha uchumi wa wakulima na uhakikisha wana chakula cha kutosha wakati wote. Takribani asilimia 75 ya wananchi maisha yao yanategemea kilimo. Aidha, sekta ya kilimo inachangia asilimia 24 ya Jumla ya Pato la Ndani – GDP. Ndiyo sababu Dira ya Taifa hadi Mwaka 2025, inasisitiza haja ya kuendeleza kilimo ili kuboresha ustawi wa wananchi, hasa wakazi wa vijijini.

Hata hivyo, sekta ya kilimo inakabiliwa na changamoto nyingi. Kubwa zaidi ni:

- Ugumu wa kupata pembejeo, gharama kubwa, na utaalumu mdogo wa kuzitumia.
- Uwekezaji mdogo katika matumizi ya teknolojia za kisasa, ikijumuisha zana za kulimia.
- Ugumu wa kupata mitaji kutoka Taasisi za Kifedha kumudu kilimo cha kisasa.
- Hali ya kutegemea mvua zisizoaminika, badala ya kujenga miundombinu za umwagiliaji.

Serikali inajitahidi kupunguza changamoto hizi kwa kushirikiana na sekta binafsi. Pamoja na jitihada hizo, suala la pembejeo feki ni tatizo kubwa linalohujumu uzalishaji wa mazao ya kilimo. Hali hii ni kubwa sana Wilayani Mbozi/ Momba. Ni miongoni mwa wilaya zinazoongoza kwa matumizi ya pembejeo bandia, au hazifikii viwango sahihi, au muda wa matumizi yake umekwisha, au vifungashio na lebo sio rasmi.

Kwa kutambua changamoto hii, ACT iliamua kushirikiana na wadau wengine kubaini athari za sheria, kanuni na taratibu mintarafu upatikanaji na matumizi ya pembejeo za kilimo Wilayani Mbozi/Momba. Ni miongoni mwa wilaya zinazoongoza nchini kwa matumizi ya pembejeo katika kilimo. Kwa ufadhili wa BEST- Dialogue, timu ya wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Kituo cha Utafiti wa Sera na Utetezi – CPRA, kwa niaba ya ACT, ilichunguza: chanzo cha pembejeo feki, kiwango / ukubwa wake, madhara yake kwa wakulima na uchumi wa Mkoa wa Songwe. Kisha kumpendekeza hatua za kuchukua ili kudhibiti uingizaji, uuzaji, usambazaji na matumizi ya pembejeo ambazo hazistahili kutumiwa.

Utafiti huo ulishirikisha wadau wengi iwezekanavyo kutoka sekta ya umma na binafsi. Baada ya kubaini tatizo na ukubwa wake, kilichofuatia ni majadiliano ya kina, hatimaye kukusanya taarifa na takwimu muhimu kutoka kwa wakulima, wataalamu, na watendaji wakuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi/Momba.

Ripoti hii inabainisha sababu za kuchakachua pembejeo na kiwango cha madhara yake. Ni matokeo ya kupitia machapisho kadhaa, pamoja nakuzungumzana wadau mbalimbali. Ripoti hii inajaribu kuweka wazi sababu za wakulima kutumia pembejeo feki na athari zake kwa ustawi wao na uchumi wa taifa. Pia watafiti wanapendekeza mabadiliko ya kisera na kimkakati kwa lengo la kuondoa au kupunguza kwa kiwango kikubwa vitendo vya kuchakachua pembejeo za kilimo. Matarajio ni kwamba, matokeo ya utafiti uliofanywa na mapendekezo yaliyotolewa, vitasaidia katika mijadala inayolenga kufanya mabadiliko katika sera, sheria na mikakati ya kudhibiti pembejeo feki.

2.0 Matokeo muhimu ya utafiti

- i. Wafanyabiashara wasio waaminifu, wakulima na baadhi ya watendaji katika Serikali, wote wanahusika katika njama za kuchakachua pembejeo za kilimo. Matokeo yake ni kwamba wakulima huwa wahanga wa njama hizo. Mbegu, mbolea na viuatilifu hafifu huwekwa katika vikasha vya plastiki au vilindo au makopo yaliyowahi kutumiwa na kuuzwa kwa bei ndogo madukani au sokoni.
- ii. Pembejeo feki huonekana zaidi nyakati ambazo matumizi ya pembejeo kwenye kilimo ni makubwa. Mathalani, katika wilaya ya Mbozi/Momba pembejeo bandia au hafifu zilizagaa sana katika msimu wa 2012/2013 wakati Serikali ilipoahidi kununua mahindi yote yatakayozalishwa.
- iii. Kiwango cha kuchakachua kiko juu sana kwenye mbegu za mahindi kwa sababu zinatumiwa na wakulima wadogo na wakubwa. Mbolea inafuatia kwa sababu udongo usipowekewa mbolea za viwandani, mavuno huwa haba sana. Matumizi makubwa ya viuatilifu ni kwenye mifugo ili kudhibiti maradhi.
- iv. Inakadiriwa kwamba asilimia 60 ya viuatilifu, na asilimia 20 hadi 30 ya mbegu zinazouzwa madukani, ni feki. Wakulima wengi huwa wahanga kwa kununua na kutumia pembejeo bandia badala ya halisi, kwa sababu siyo rahisi kuzipambanua. Hii ni miongoni mwa sababu za kuambulia mavuno haba na hafifu.
- v. Matokeo ya kutumia pembejeo feki ni kwamba katika msimu wa 2012/2013 mavuno ya mahindi yalipungua kutoka magunia 25 hadi 8 kwenye eka moja. Kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya hutoza ushuru wa Shs. 1,000 kwa kila gunia la mahindi au maharage, maana yake ni kwamba pato la wilaya kutokana na ushuru lilipungua sana.
- vi. Kuongezeka kwa pembejeo feki ni pigo kubwa kwa wakulima wadogo wanaojitahidi kujikwamua kwenye umaskini. Kilimo ni mhimili mkuu wa ustawi wa familia zinazoishi vijijini. Mapato yatokanayo hutumiwa kukidhi mahitaji muhimu, kama afya ya wanakaya na karo ya shule.

- vii. Utafiti huu ulibaini aina mbili za wahusika. Aina ya kwanza ni watengenezaji, wasambazaji na wauzaji wa pembejeo. Aina ya pili ni watendaji kwenye Halmashauri na Wizara husika, vyombo vya ulinzi na usalama, na wakulima wenyewe.

Kulingana na malengo mahususi ya utafiti uliofanyika, kuna mambo kadhaa yaliyobainika. Ufuatao nimhutasari wake:

- Pembejeo feki na zilizo hafifu ambazo zimezagaa sehemu zote wilayani Mbozi, zina athari mbaya kwa kilimo.
- Athari hasi zinaonekana wazi kutokana nahali ya kudumaa kwa uchumi na ustawi wa wananchi.
- Hali mbaya ilifikia kilele mwaka 2012 / 2013 wakati matumizi ya pembejeo feki yalipongezeka ghafla.
- Kuna mwamko na utashi miongoni mwa wadau wa kujadili na kuamua namna ya kukabili changamoto hii.

KUNDI	CHANGAMOTO
Wakulima	<ul style="list-style-type: none"> • Uelewa mdogo wawakulima kutambua pembejeo halisi na zisizo halisi. Hasa wale ambao hawajui kusoma maandishi kwenye lebo. • Umaskini unaosababisha wakulima kuchagua kununua bidhaa za bei nafuu, hata kama wana wasiwasi na uadilifu wa muuzaji. • Kutoelewa vizuri jinsi ya kutumia pembejeo kwa usahihi.
Wafanyabiashara	<ul style="list-style-type: none"> • Kutokuwa na maadili katika kazi zao, hivyo kuwa na tamaa ya kupata faida kubwa kwa njia haramu. • Udhaifu wa sheria, kanuni na taratibu za kubaini wahalifu na kuchukua hatua stahiki. • Kuwepokwa pembejeo feki madukani zinazotoka nchi za jirani, na kusababisha wafanyabiasharawenyeji kuza bidhaa nyingine.
Serikali	<ul style="list-style-type: none"> • Udhaifu katika kufuatilia na kutathmini utaratibu wa kuhakiki ubora wa pembejeo za kilimo. • Rushwa iliyokithiri inayodaiwa na watendajiambayo kusababisha ugumu wa kunasa wahalifu. • Uhaba wa Maafisa Wakaguzi wa pembejeo, pamoja na nuchache wa nyenzo za kufanyia kazi. • Kutofanyika tafiti za kutosha kuhusu kiasi na aina ya pembejeo zinazohitajiwa na wakulima.

Kwa jumla, pembejeo feki mkoani Songwe ni tatizo kubwa sana, na athari yake ni kubwa mno. Hasa kwa wakulima wadogo. Kwa hiyo, ni muhimu kuchukua hatua stahiki za kudhibiti tatizo hili, kila chombo / taasisi kwa nafasi yake.

3.0 Muhtasari wa Mapendekezo

- Kuandaa kampeni za kuongeza mwamko na uelewa miongoni mwa wadau, kwa njia ya semina, safari za mafunzo, vipeperushi na makala/ taarifa maalumu kwenye magazeti.
- Kuandaa mashamba yenye mapando ili kuonyesha matokeo ya kutumia pembejeo zilizo sahihi.
- Kuhakikisha pembejeo zinafikishwa karibu na wakulima, na wanazipata kwa wakati muafaka, na kwa bei nafuu.
- Kuweka pembejeo kwenye vifungashio vidogo (mathalani kilo 1 hadi 5) ambazo wakulima wadogo wana uwezo wa kuzinunua.
- Kuhakikisha wakulima wanaunganishwa na Wataalamu wa Kilimo, pia wanapata huduma za ugani kila wanapozihitaji.
- Kushirikiana na Vyama vya Hiari – NGO kuwajengea uwezo wakulima, na kuwasaidia kupata soko la mazao yao.
- Wakulima kupewa elimu stahiki kuhusu kiteknolojia mpya, kwa njia ya machapisho (*bila kuyalipia*) katika lugha wanayoielewa.

Kwa msingi wa utafiti wa awali uliofanyika, watafiti wanashauri hatua za kuchukua ili kudhibiti pembejeo feki, na akina nani watahusika.

UWAJIBIKAJI WA JUMLA KWA LENGU LA KULETA MABADILIKO

SUALA	MABADILIKO YANAYOTAKIWA	WAHUSIKA
Kuongeza uelewa wa wakulima	<ul style="list-style-type: none"> • Kuimarisha vyama / vikundi vya wakulima • Wadau kushirikiana kuweka mikakati ya kuwezesha wakulima kupata taarifa kuhusu upatikanaji wa pembejeo halisi, na mafunzo. 	<p><i>Vyama vya wakulima Idara ya Kilimo ADP - Mbozi</i></p>
Kuongeza uwezo wa kuzalisha mbegu	<ul style="list-style-type: none"> • Kuandaa mikakati ya kuimarisha ubia baina ya sekta binafsi na umma katika kutengeneza, kusambaza na kupromoti pembejeo. • Serikali kusaidia sekta binafsi kupata mitaji ya kujenga miundombinu ya kusindika mbegu ambayo imejengwa 	<p><i>Vyama vya wakulima Wazalishaji wa mbegu Idara ya Kilimo ADP – Mbozi</i></p>

	kwenye sehemu muafaka.	
Kuboresha mtandao wa kusambaza mbegu	<ul style="list-style-type: none"> • Kuongeza uwezo wa wasambazaji na wauzaji wa pembejeo ili shughuli hiyo ifanyike kwa ufanisi zaidi na kupunguza gharama. • Kutoa elimu kwa wafanyabiashara waaminifu kuhusu faida ya kuuza pembejeo halisi, na kutumia vifungashio na lebo zilizo sahihi. 	<i>Vyama vya wakulima Wauzaji wa mbegu Maafisa Ugani ADP – Mbozi</i>
Bei za mazao	<ul style="list-style-type: none"> • Kuboresha utaratibu wa kupata taarifa za soko la mazao. Pamoja na kutumia Teknolojia ya Kisasa – ICT ya kupashana taarifa hadi vijijini 	<i>Vyama vya wakulima Idara ya Kilimo ADP - Mbozi</i>
Masuala la kitaasisi	<ul style="list-style-type: none"> • Kutambua faida ya kushirikiana na kupromoti mahusiano mazuri na sekta isiyo rasmi. 	<i>Vyama vya wakulima Wafanyabiashara Idara ya Kilimo ADP – Mbozi</i>
Uwezo wa washikaduu	<ul style="list-style-type: none"> • Kubaini maeneo ambayo yanahitaji kuongezewa uwezo kiutendaji. • Kuweka kipengele cha “kuongeza uwezo wa wadau” katika shughuli za baadae. 	<i>Vyama vya wakulima Wafanyabiashara Idara ya Kilimo ADP – Mbozi</i>

MAJUKUMU MAALUM NA WAHUSIKA WAKE

HATUA ZA KUCHUKUA	WAHUSIKA WAKUU
1. Kuandaa orodha ya wauzaji wa pembejeo za kilimo. Jina la muuzaji, anuani, aina ya pembejeo, eneo ambalo anatoa huduma hii.	<i>Afisa Kilimo wa Wilaya</i>
2. Kuelekeza watengenezaji na wafungashaji wa pembejeo kuweka bidhaa zao katika makasha madogo ambayo wakulima wenye uwezo mdogo watamudu.	<i>Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya</i>
3. Kuendesha mafunzo kwa wakulima kuhusu jinsi ya kutumia pembejeo kwa usahihi / tija. Zoezi hili lifanyike angalau mara moja kwa mwa kwenye ngazi ya kata.	<i>Afisa Kilimo wa Wilaya Afisa Mtendaji wa Kata</i>

4. Kufanya ukaguzi wa pembejeo za kilimo madukani kwa kustukiza. Yaani bila kutoa taarifa ya awali.	<i>Afisa Kilimo wa Wilaya</i>
5. Kuonyesha jinsi ya kutumia pembejeo kwa usahihi, na kuandaa mashamba ya majaribiokatika kila tarafaili kuthibitisha matokeo tarajiwa ya kutumia pembejeo.	<i>Afisa Kilimo wa Wilaya</i>
6. Kuandaa vikundi vya wakulima mahiri katika kila kijiji.	<i>ADP – Mbozi na Afisa Mtendaji wa Kijiji</i>
7. Kuwezesha na kuhakikisha vikundi hivyo vinafundisha wakulima wengine.	<i>Vikundi Mahiri vilivyoanzishwa</i>
8. Kuchagua wauzaji wa pembejeo wachache ambao wana rekodi nzuri kwa uaminifu na uadilifu.	<i>Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya Afisa Kilimo wa Wilaya Wafanyabiashara na Wakulima</i>
9. Kuweka utaratibu wa kutoa ripoti kuhusu hali ya pembejeo feki kwenye wilaya, kila mwezi.	<i>Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya Afisa Mtendaji wa Kata Jeshi la Polisi Wawakilishi wa wakulima</i>
10. Kuhakiki / kuthibitisha usahihi wa ripoti kwenye ngazi ya kijiji, kwa kushirikisha vikundi vya wakulima mahiri	<i>Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya Afisa Mtendaji wa Kata Wawakilishi wa wakulima</i>
11. Kuaandaa na kuchapisha makala zinazoeleza mafanikio ya kutumia pembejeo za kilimo zilizo halisi ndani ya wilaya, na kwingineko.	<i>Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya</i>

MWISHO

